

NOT FOR SALE



UNYUNYIZIAJI
Owalo asifu mradi
wa unyunyiziaji
wa Maragua kama
wenye tija
UK 7



USKAUTI
Kaunti ya Nyeri
yatambuliwa kimataifa
kama kitovu cha
uskauti.
UK 14

UTAFITI
Egerton yazindua
mbegu zenye
mavuno mengi na
zinazostahimili
ukame.

MyGov.

www.mygov.go.ke

Aprili 1, 2025

TATHMINI YAKO YA WIKI

TOLEO No. 38/2024-2025



UK 28

Takwimu za Wiki

500,000

Jumla ya wanafunzi waliojiandikisha katika taasisi za kiufundi nchini

Kenya katika Mashindano ya Kimataifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) ya Huawei.

598B

Kiasi cha pesa ambacho Serikali itakusanya ili kupanua eneo la unyunyiziaji kwa ekari milioni moja katika kipindi cha miaka 10 ijayo.

60M

Kiasi cha pesa ambacho Idara ya Habari imeomba kutoka kwa Serikali ya Kitaifa kwa bajeti ya matumizi ya mara kwa mara katika MDAC zote ili kugharamia shughuli

1.5M

Tani za mbolea ambazo serikali itaagiza kulingana na Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Mbolea, Haron Khator.

500

Idadi ya watu katika Kaunti ya Wajir walioambukizwa na ugonjwa hatari wa kala-azar tangu Septemba mwaka jana.

3

Wanafunzi kutoka JKUAT watakaoiwakilisha

Serikali yatoa mifuko milioni 1 ya mbolea kutatua upungufu



Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Mbolea, Haron Khator, anamkabidhi mkulima wa Thika mbolea ya ruzuku aliyoinunua katika Bodi ya Kitaifa ya Nafaka na Mazao mjini Thika siku ya Jumanne, Machi 25, 2026.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Mbolea, Haron Khator, asema kuweka idadi ya mifuko ya mbolea inayotolewa kwa ruzuku ambayo mkulima anaweza kununua kutoka kwa bodi ya nafaka husaidia kuzuia magenge kununua kwa wingi ili kuuza tena

NA MUOKI CHARLES, KNA

Wakulima watakuwa na mbolea ya kutosha huku mvua za masika zikiendelea, licha ya wasiwasi kwamba mbolea zilizohifadhiwa katika bodi za nafaka huenda zisiweze kukidhi mahitaji.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Mbolea, Haron Khator, amesema kwamba angalau magunia milioni moja ya mbolea yameachiliwa kutoka Bandari ya Mombasa kwa ajili ya kusanafirishwa hadi maeneo ya mashambani.

1.5M

Tani zaidi za mbolea ambazo serikali imeagiza kutoka nje ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka

ENDELEA UK 2

Serikali kuunganisha mifuko ya Uwezo, Vijana, na ule wa Wanawake kuwa mfuko wa Biashara



Waziri wa Ushirika na MSMEs Wycliffe Oparanya



NA JOHN OCHANDA, KNA

Serikali itaunganisha Hazina ya Uwezo, Hazina ya Vijana, na Hazina ya Biashara ya Wanawake kuwa chombo kimoja ili kurahisisha upatikanaji wa fedha kwa biashara ndogo ndogo. Waziri wa Ushirika na Biashara Ndogo na za Kati (MSMEs), Wycliffe Oparanya, amesema kwamba kuanzishwa kwa Hazina ya Biashara kutafunga mianya iliyosababisha matumizi mabaya ya fedha hizo. Akizungumza katika Kaunti Ndogo ya Khwisero wakati wa ugawaji wa fedha za Uwezo, Waziri Oparanya alisema kuwa hatua ya kuunganisha hazina hizi inalenga kuongeza ufanisi, kuboresha ugawaji wa rasilimali, na kuzuia watu wa-

chache kunufaika mara nyingi kutoka kwa hazina tofauti. Oparanya alieleza wasiwasi wake kuwa baadhi ya vijana na wanawake wamekuwa wakitumia mfumo huu uliogawanyika kupata mikopo mingi, hivyo kuwanyima wengine fursa ya kunufaika. "Tuna visa ambapo mwanamke anafanya maombi ya Hazina ya Biashara ya Wanawake, kisha anachukua Hazina ya Vijana, na baadaye anaungana na kikundi cha kujisaidia kupata Hazina ya Uwezo. Hii ni dhuluma kwa mfumo huu, ilhali wengine wengi wanahitaji msaada wanaachwa nje," alisema Oparanya.

ENDELEA UK 2

Serikali yatoa mifuko milioni 1 ya mbolea kutatua upungufu

ENDELEA KUTOKA UK 1

Ameongeza kuwa serikali pia imegiza uingizaji wa tani milioni 1.5 zaidi za mbolea. Khator, ambaye pia ni Katibu wa Utawala katika Idara ya Kilimo, alizungumza wakati wa ukaguzi wa ghala la Bodi ya Kitaifa ya Nafaka na Mazao (NCPB) mjini Thika, Kaunti ya Kiambu. Alieleza kuwa kuweka ukomo wa idadi ya magunia ya mbolea yenye ruzuku ambayo mkulima anaweza kununua kutoka kwa bodi ya nafaka kunasaidia kuratibu usambazaji na kuzuia magenge ya walanguzi kununua kwa wingi ili kuuza kwa bei ya juu. “Kuweka kikomo kwa idadi ya magunia yanayouza kwa mkulima si isihara ya uhaba wa mbolea, bali ni hatua ya kurahisisha usambazaji wake. Tuna akiba ya kutosha kuendeleza msimu huu wa upanzi,” alisema Khator. Wakati huo huo, alikiri kuwa kasi ya usambazaji wa mbolea kwa wakulima ni polepole kutokana



Wakulima wamiminika katika Bodi ya Nafaka na Mazao ya Taifa ya Thika kununua mbolea ya ruzuku kwa ajili ya msimu wa upanzi

na mahitaji makubwa. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, alisema kuwa NCPB imeajiri wafanyakazi wa muda wa ziada katika vituo vya usambazaji ili kuharakisha mchakato huo. “Tunatambua kuwa wakulima wameeleza wasiwasi kuhusu ucheleweshaji wa usambazaji wa mbolea. Hata

Tunawasihi NCPB kuharakisha mchakato wa usambazaji

hivyo, wakati mwingine wafanyakazi wa NCPB hulemewa na idadi kubwa ya wakulima wanaotafuta mbolea. Tumeongeza nguvu kazi na tunatumiwa tatizo hili litapatiwa suluhisho,” alisema. Khator pia aliwahakikishia wakulima kuwa NCPB inashirikiana na mashirika mengine kuzuia mbolea bandia kuingia sokoni. Aliwashauri wakulima wasihofu wanapokutana na mbolea zenye rangi tofauti na zile walizozoea, akieleza kuwa mchanganyiko mpya wa mbolea unaundwa kwa utafiti.

“Mbolea hupitia majaribio na uchunguzi wa kina ili kuhakikisha kuwa wakulima wanapata bidhaa za ubora wa juu pekee. Tunawahimiza pia wakulima kuripoti ikiwa watahuku uwepo wa mbolea bandia. Msihofu kuhusu tofauti za rangi, kwani mchanganyiko mpya umetengenezwa mahsusi kwa mazao na kazi fulani,” alifanua. Wakulima wakiongozwa na Patrick Njui walieleza kufurahishwa kwao na mbolea ya bei nafuu inayouza kwa Sh2,500 kwa kila gunia la kilo 50 kutoka kwa maduka ya serikali. Hata hivyo, walibainisha kuwa wengi wao wamekuwa wakinogojia kwa wiki kadhaa kupokea mgao wao. Wengi pia walilalamikia kupokea magunia machache kuliko walivyotarajia. Wakulima hao walieleza matumaini yao kuwa mpango wa serikali utaboresha uzalishaji wao wa kilimo, wakisema kuwa tangu kuanzishwa kwa mbolea ya ruzuku, mavuno yao yameongezeka.

Serikali kuunganisha hazina ya Uwezo, Vijana, na Wanawake kuwa mfuko wa Biashara


ENDELEA KUTOKA UK 1

Aliongeza kuwa Hazina ya Biashara itaziba miya hii kwa kuanzisha hifadhidata moja kuu itakayofuatilia na kuhibiti wanufaika, ili kuhakikisha usambazaji wa rasilimali kwa haki. Hazina ya Biashara itatoa mikopo nafuu, programu za kujengea uwezo, na ushauri kwa vijana, wanawake, na wamiliki wa biashara ndogo ndogo kote nchini. Kwa kuunganisha hazina hizi, Oparanya alisema kuwa serikali inalenga kurahisisha upatikanaji wa fedha, kupunguza urasimu, na kuzuia marudio ya ufadhili kwa watu walewale. “Serikali inaziunganisha hazina hizi chini ya Hazina ya Biashara ili kuanzisha mfumo bora zaidi na kifedha, wenye uwazi na athari chanya kwa biashara ndogo ndogo,” alisema Oparanya. Viongozi kadhaa wa Magharibi waliohudhuria, wakiwemo Wabunge Christopher Aseka (Khwisero), Bernard Shinali (Ikolomani), Emmanuel

Wangwe (Navakholo), Fred Ikana (Shinyalu), Elsie Muhanda (Kaunti ya Kakamega), na Titus Khamala (Lurambi), waliunga mkono pen-dekezo hilo, wakisema litasaidia kukuza biashara za wenyeji na kuimarisha uchumi. Mbunge wa Khwisero, Christopher Aseka, alisema kuwa hatua hiyo inalingana na juhudi za serikali za kuimarisha ujasiriamali na kuunda nafasi za kazi endelevu. “Kwa kuunganisha hazina hizi, tunapunguza uzembe na kuhakikisha kila mfiyabishara, hasa vijana na wanawake, wanapata mtaji kwa urahisi zaidi,” alisema Aseka. Mbunge wa Navakholo, Emmanuel Wangwe, alisema usimamizi mzuri na uwazi vitakuwa muhimu kwa mafanikio ya hazina hiyo. Serikali inatarajiwa kuzindua rasmi Hazina ya Biashara katika miezi ijayo, ikiwa na miongozo wazi kuhusu masharti ya ulipaji.



**KENYA
WILDLIFE
SERVICE**



INVITATION TO TENDER

KWS is inviting interested and eligible national candidates to tender for the following:

NO.	TENDER REFERENCE NO.	TENDER NAME	ELIGIBILITY	BID SECURITY
1.	KWS/ONT/HRA/65/2024-2025	PROVISION OF COMPREHENSIVE GROUP MEDICAL INSURANCE COVER FOR BOARD OF TRUSTEES AND STAFF	OPEN TO ALL	5,000,000

Tender documents containing detailed specifications and requirements can be downloaded for free at KWS website: www.kws.go.ke and the Public Procurement Information Portal; <https://www.tenders.go.ke/web-site>; Interested candidates may seek further information from the Procurement Office at KWS Headquarters between 8 am-1 pm & 2 pm-5 pm during weekdays, Tel. 020-2379407-15 Cell: 0726610508/9, or email: director@kws.go.ke; hps@kws.go.ke

All clarifications and/or amendments will be published on the KWS website and tenderers are required to check for any addendums or amendments in the course of the bidding period before the closing date.

An original tender Security must accompany all Tenders indicated above and be valid for 126 days from the date of tender opening, in the form of a bank guarantee from a reputable bank recognized by the Central Bank of Kenya or an Insurance Company payable to the Director General Kenya Wildlife Service. (Self-insured tender securities are not allowed)

The completed bids in plain sealed envelopes marked with the tender reference number and tender name shall be deposited into the Tender Box located at the entrance of **Main Reception, KWS Headquarters, Langata Road P.O. Box 40241-00100, Nairobi** on or before **Tuesday, 8th April, 2025 at 11.30 am EA**.

Tenders shall be opened immediately thereafter in the presence of bidders' representatives who wish to attend at the KWS Vet Board Room.

Further information is available at www.kws.go.ke and the PPIP portal; <https://www.tenders.go.ke/website>

DIRECTOR GENERAL



**THE NATIONAL
TREASURY & ECONOMIC
PLANNING**

REPUBLIC OF KENYA



PUBLIC NOTICE

ROLLOUT OF THE ELECTRONIC GOVERNMENT PROCUREMENT SYSTEM

NOTICE TO ALL SUPPLIERS, CONTRACTORS & CONSULTANTS

The National Treasury is rolling out an end-to-end Electronic Government Procurement (e-GP) System to all Procuring Entities in both the National and County Governments. This is one of the public finance management reforms that is geared towards efficiency and value for money in public procurement. The e-GP system rollout is in line with the directive by His Excellency, the President in his State of the Nation address on 21st November, 2024 that the National Treasury rolls-out the e-GP system by the first quarter of 2025.

The implementation and use of the e-GP system will result in reduced cost of goods, works and services; increased transparency in procurement processes and practices; improved efficiency in procurement by minimizing the procurement cycle time; maximization of value for money; accountability; improved confidentiality, integrity and authenticity of transactions between procuring entities and suppliers; streamlined procurement procedures across the government through standardization of processes and practices; and enhanced procurement information management that will facilitate procurement planning, monitoring, evaluation and reporting.

Suppliers/Contractors/Consultants are required to self-register on the e-GP portal that is accessible through www.egpkenya.go.ke. In addition, they are requested to note the following:

- Suppliers/Contractors/Consultants may contact the support address indicated below in case of challenges faced during registration: Email address: support@egpkenya.go.ke Telephone: **+254 (020) 3341030/3340400/3340433**;
- Suppliers/Contractors/Consultants within Nairobi may visit e-GP offices situated on **6th Floor, Room 622 Treasury Building, Harambee Avenue** to receive registration assistance between 9.00 a.m.- 4.00 p.m;
- Suppliers/Contractors/Consultants may also visit The National Treasury desk in all Huduma Centres during the office working hours;
- Supplier Registration Module Manual is available on the e-GP Portal; and
- The National Treasury will organize weekly supplier registration webinar every Thursday commencing **10th April 2025 to 30th May 2025**. Suppliers will be required to register for training through links provided on www.egpkenya.go.ke under Supplier Training. Only suppliers who have registered for training will be invited to the webinar.

**DR. CHRIS KIPTOO, CBS
PRINCIPAL SECRETARY/ THE NATIONAL TREASURY**

Jaji Koome azindua mkakati mpya kukabili rushwa katika Mahakama

NA CLINTON NG'IELA NA NICHOLAS KIGONDU (PCO)

Kenya imechukua hatua muhimu katika mapambano dhidi ya ufisadi kwa kuzindua Mfumo wa Kimkakati wa Mwongozo wa Kupambana na Ufisadi katika sekta ya haki. Akizungumza jijini Nairobi wakati wa uzinduzi huo, Jaji Mkuu (CJ) Martha Koome alisisitiza kuwa mpango huu unaashiria mwanzo wa sura mpya yenye uthabiti katika dhamira ya pamoja ya kudumisha uadilifu, uwajibikaji, na haki. Jaji Mkuu alisema kuwa mfumo huu, uliotayarishwa chini ya Baraza la Kitaifa la Usimamizi wa Haki (NCAJ), unatoa mikakati ya muda mfupi, wa kati, na mrefu ya kutokomeza ufisadi ndani ya mfumo wa haki. Koome pia alifichua kuwa mfumo huu uliongozwa na maazimio yaliyofikiwa katika Mkutano wa Wakuu wa Mihimili ya Serikali, ulioitishwa na Rais William Ruto mnamo Januari 2024 katika Ikulu, Nairobi. “Ufisadi ni changamoto kubwa inayodhoofisha im-



Jaji Mkuu Martha Koome akizungumza wakati wa uzinduzi wa Mfumo wa Mkakati wa Mwongozo wa Kupambana na Ufisadi wa Baraza la Kitaifa la Usimamizi wa Haki (NCAJ) kwa Sekta ya Haki katika hoteli moja jijini Nairobi.

ani ya umma na kudhoofisha taasisi zetu,” Koome alisema, akiwahimiza wadau wote kutekeleza mfumo huu kikamilifu. Aidha, alisisitiza kuwa ushirikiano kati ya mashirika mbalimbali ni muhimu katika kukabiliana na ufisadi na kurejesha imani katika sekta ya haki. Jaji Mkuu pia alieleza kuwa Idara ya Mahakama imeanzisha Kamati za Uadilifu wa Mahakama katika kila mahakama ili kushughulikia ufisadi

katika ngazi ya chini. “Nimeagiza mahakama zote kufanya mikutano ya asubuhi kila siku ili kuthibitisha kuwa hakuna ada ya urasimu inayohitajika kwa utoaji wa haki,” alitangaza. Zaidi ya hayo, Koome alieleza kuwa mfumo huu wa mwongozo unajumuisha mipango 76 inayolenga kuimarisha uongozi wa maadili na kuhakikisha mageuzi madhubuti ya kisheria. “Acha mkakati huu uwe

nyenzo hai inayosukuma mabadiliko halisi,” alisema Koome, akibainisha kuwa mafanikio ya mpango huu yatategemea utashi wa kisiasa, ushiriki wa umma, na ugawaji sahihi wa rasilimali. Kwa mujibu wa maelezo yake, Jaji Mkuu alisisitiza kuwa mfumo huu ni ramani ya njia ya kuimarisha uadilifu na uwajibikaji katika sekta ya haki, huku akihakikisha dhamira ya Idara ya Mahakama kwa kutoa mifano ya Kamati za Uadilifu wa Mahakama na mikutano ya kila siku ya mahakama ili kuhakikisha uwazi. Ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa mfumo huu, Koome alihimiza mashirika yote ya serikali kuimarisha ahadi zao kwa majukumu yao ya kikatiba na kushirikiana katika vita dhidi ya ufisadi. Alisisitiza umuhimu wa kutenga rasilimali za kutosha kutoka kwa Hazina ya Kitaifa ili kusaidia juhudi za kupambana na ufisadi na akaitaka Bunge kutekeleza mageuzi ya kisheria yaliyotajwa katika mfumo huo.

Serikali yaahidi ugavi usiokatizwa wa ARV licha ya kupunguzwa kwa ufadhili wa USA

NA GEOFFREY SATIA

The Serikali itahakikisha upatikanaji wa ARVs kwa uhakika ili kulinda kinga za walioambukizwa HIV, Waziri wa Afya anayeondoka, Deborah Mlongo Barasa, amesema. Dkt. Barasa alisisitiza kuwa serikali haitaruhusu wagonjwa wa HIV kuteseka kutokana na changamoto za usambazaji wa dawa, akihakikishia kuwa vituo vyote vinavyotoa ARVs vitapokea mahitaji yao ipasavyo. Waziri alitoa kauli hiyo wakati wa maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Afya ya Kinywa Duniani katika viwanja vya Chuo cha Mafunzo ya Tiba cha Mosoriot, Kaunti ya Nandi, eneo la Chesumei. Ahadi hii inatolewa licha ya kusitishwa kwa ufadhili wa Shirika la Marekani la Maeleleo ya Kimataifa (USAID) na serikali

ya Marekani, ambalo kwa muda mrefu limekuwa na jukumu muhimu katika kusambaza ARVs kwa nchi zinazozitaji. Tangazo la serikali ya Marekani lilizua hofu miongoni mwa Wakenya wanaotegemea ARVs, wengi wao wakiwa na wasiwasi juu ya hatima ya maisha yao. “Kama serikali, tumejitolea kuhakikisha kuwa hakuna mgonjwa anayepata changamoto ya upatikanaji wa ARVs, hivyo hakuna haja ya kuwa na wasiwasi,” alisisitiza. Dkt. Barasa aliwataka wakazi wa Nandi kutilia maanani afya ya kinywa, akionya kuwa tatizo hilo linaweza kiongoni mwa Wakenya. Alihimiza wakazi kunufaika na Kituo Kipya cha Meno kilichoanzishwa katika Chuo cha KMTC Mosoriot ili kuboresha afya ya kinywa.



INVITATION TO TENDER

Kenya Power invites tenders from interested bidders for provision of the following:-

NO.	TENDER NO.	ITEM DESCRIPTION	TENDER COMMENCEMENT DATE	PRE-BID MEETING	TENDER CLOSING DATE
1.	KP1/9A.2/OT/042/LS/24-25	Outsourcing Scanning Services of Records	Wednesday 02.04.2025	Thursday 10.04.2025 at 10.30 a.m. (Stima Plaza Auditorium)	Tuesday 22.04.2025 at 11.00 a.m.
2.	KP1/9A.2/OT/037/NM/24-25	Rehabilitation of Transmission Lines – Design, Supply and Construction	Thursday 03.04.2025	Monday 14.04.2025 10.00 a.m. - 12.00 p.m. Site Visit (See below)	Thursday 15.05.2025 at 10.00 a.m.

TENDER NO. 2 - KP1/9A.2/OT/037/NM/24-25

DATE	SITE VISIT
15.04.2025	Nairobi North – Cianda 66 (132 kV) Line Meeting Point at Nairobi North 220kV S/S
17.04.2025	Kiganjo – Nanyuki 132kV Line Meeting Point at Chaka Town
18.04.2025	Olkaria1 AU/Naivasha 132 kV Line Meeting Point at Olkaria II 220 kV Substation
21.04.2025	Musaga – Webuye 132kV Line Meeting Point at Webuye 132 kV Substation
24.04.2025	Juja – Rabai 132kV Line Meeting Point at Voi 132 kV Substation

Tender documents detailing the requirements of the above tenders may be obtained from the Kenya Power website (www.kplc.co.ke) from the dates shown above.

**GENERAL MANAGER
SUPPLY CHAIN & LOGISTICS**

www.kplc.co.ke

DIAL *977# | Access Kenya Power services fast and easy

www.kplc.co.ke | Customers@kplc.co.ke | Kenya Power | www.kplc.co.ke | 0777 | 0709-070 707, 0753-170 170



TENDER NOTICE

The Kenya Power Pension Fund invites firms for the following:

NO.	TENDER NAME	TENDER NUMBER	ELIGIBILITY	TENDER CLOSING DATE
1.	PROVISION OF STRATEGIC DEVELOPMENT CONSULTANCY SERVICES	KPPF/PROC/2-E/01/2025	OPEN	Wednesday 30 th April 2025 at 11.30AM
2.	THREE YEAR FRAMEWORK AGREEMENT FOR PROVISION OF CONFERENCE AND HOTEL SERVICES	KPPF/PROC/2-A/01/2025	OPEN	Wednesday 23 rd April 2025 at 11.30AM
3.	PROVISION OF LEGAL AND GOVERNANCE AUDIT SERVICES	KPPF/PROC/2-A/02/2025	OPEN	Wednesday 16 th April 2025 at 11.30AM

Tender documents detailing the requirements of the above tender may be downloaded from Kenya Power Pension Fund website www.kppf.co.ke from **Tuesday 1st April 2025 at no fee**. Bidders are required to register by sending an email to tenders@kppf.co.ke in order to receive clarifications and/or communication, where necessary.

Completed Tender Documents in plain sealed envelopes clearly marked with tender name and tender number should be addressed as follows: -

**CEO & TRUST SECRETARY
Kenya Power Pension Fund,
Stima Plaza Annex, Kolobot Road, Parklands
P.O Box 1548 – 00600
Nairobi, Kenya.**

and deposited in the Tender box at Ground floor, Stima Plaza Annex next to the Lift Lobby

So as to be received on or before the closing dates shown above. Tenders will be opened promptly thereafter in the presence of the Tenderer's or their representatives who choose to attend in Kenya Power Pension Fund at Stima Plaza Annex ground floor, Kolobot Road, Parklands, Nairobi.

Save for responding to KPPF's request for clarification, bidders shall not contact or discuss any aspect of their tenders with KPPF after tender closing date and before receipt of notification of award of tenders or letters of regret, as applicable. Any such contact shall lead to disqualification of the tenderer.

CEO & TRUST SECRETARY.



Wakulima kufaidika huku Serikali ikiongeza ufadhili wa kilimo

NA ANITA OMWENGA, KNA

Serikali imeongeza ufadhili wa kilimo kwa Sh3.8 bilioni ili kusaidia mifumo ya chakula na kilimo kwa njia endelevu nchini. Katibu wa Wizara ya Kilimo, Dkt. Kipronoh Ronoh, alisema kuwa mgao wa sasa wa fedha kwa sekta ya kilimo umeongezeka hadi Sh77.7 bilioni, kutoka Sh73.9 bilioni katika mwaka wa kifedha uliopita. Ongezeko hili linatarajiwa kuimarisha mnyororo mzima wa thamani wa kilimo—kutoka uzalishaji hadi upatikanaji wa masoko—huku likiboresha usalama wa chakula na kuongeza fursa za ajira. Alisisitiza kuwa wadau wote wa mnyororo wa thamani wa kilimo, hasa wakulima ambao ndio wadau wakuu wa sekta hiyo, wanahitaji ufadhili ili kununua pembejeo muhimu za kilimo kama vile mbegu na mbolea, kukodisha ardhi ya ziada ya kilimo, kununua mifugo, na kugharamia mavuno na masoko. Ronoh alibainisha kuwa ongezeko hili la ufadhili linalenga kuboresha uzalishaji endelevu wa mifumo ya chakula na kilimo, kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno, na kuwawezesha wakulima wadogo, hasa wanawake na vijana.

“Katika mwaka uliopita,



Katibu wa Kilimo Dkt. Kipronoh Ronoh akihutubu wakati wa uzinduzi wa FINAS 2025 Dialogue Summit jijini Nairobi

serikali imekuwa ikiwaunga mkono wakulima kwa kuboresha upatikanaji wao wa pembejeo kama mbolea, huduma za ugani, na mechanization ya kilimo,” alisema. Ronoh alitoa matamshi haya wakati wa uzinduzi wa vyombo vya habari wa Mkutano wa Mazungumzo ya Ufadhili Endelevu wa Mifumo ya Chakula na Kilimo (FINAS) 2025, ambao umepangwa kufanyika Mei mwaka huu. “Katika wakati ambapo serikali za Afrika zinazidi kujitolea kwa mifumo ya ufadhili wa kujitegemea, Mazungumzo ya FINAS 2025 yanakuwa jukwaa muhimu la kufikiria upya ufadhili wa mifumo ya chakula na kilimo kupitia mifano bunifu, mabadiliko ya kidijitali na

ushirikiano wa kimkakati,” alisema Ronoh. Alisema kuwa wizara inaendelea kuipa kipaumbele utekelezaji wa programu na sera zinazolenga kufanikisha matarajio yaliyoainishwa chini ya Ajenda ya Uchumi wa Chini Kiu-nuka (BETA) ya serikali, inayolenga kufanikisha usalama wa chakula, kupunguza uagizaji wa chakula kutoka nje, na kuongeza mauzo ya nje. Aliongeza kuwa BETA inazingatia ushirikiano wa kimuundo na sekta binafsi kupitia mipango kama mazungumzo ya FINAS. “Majukwaa haya yanatoa fursa ya kuonisha juhudi za wadau na kufuatilia maendeleo. Tunasalia thabiti katika dhamira yetu ya kushirikiana na se-

кта binafsi katika kubadilisha mifumo ya chakula na kilimo,” alisema. Katibu Mkuu alifichua kuwa ufadhili endelevu wa kilimo umetokana na mazungumzo ya FINAS 2024. Mfumo huu unalenga kuboresha matumizi ya fedha za umma ili kusaidia maendeleo ya mifumo ya chakula nchini Kenya. “Mkutano ujao wa FINAS unatoa jukwaa na fursa ya kuchunguza suluhisho bunifu za kifedha na njia za kuhakikisha ukuaji na uendelevu wa mifumo ya chakula na kilimo barani Afrika,” alisema. Katibu Mkuu alibainisha kuwa mazingira ya ufadhili wa kimataifa yanabadilika, na sekta ya kilimo ni moja ya sekta zilizoathiriwa kwa kiasi kikubwa na mabadiliko ya sera kutoka kwa wadau wa maendeleo. Alisema serikali inatafuta suluhisho bunifu kama vile ufadhili wa mchanganyiko, hati fungani za kijani, fedha za wahamiaji wa diaspora, matumizi ya rasilimali za ndani, na ushiriki mkubwa wa sekta binafsi ili kuziba mapengo haya ya kifedha. “Kwa kukumbatia mifano hii, tunaamini tunaweza kuhakikisha ustahimilivu na uhai wa mifumo yetu ya chakula na kilimo,” alisema, akiongeza kuwa hali hii inailazimu serikali kufikiria upya mifumo yake ya ufadhili na uwekezaji iliyopo.

Kirinyaga yazindua X-Ray inayoendeshwa na AI kuboresha uchunguzi wa Kifua Kikuu

NA MUTAI KIPNGETICH, KNA

Serikali ya Kaunti ya Kirinyaga imezindua mfumo wa kidijitali wa X-Ray unaotumia akili bandia (AI) ili kuboresha utambuzi wa mapema na matibabu ya kifua kikuu (TB). Uzinduzi wa kifaa hiki kipya wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kifua Kikuu Duniani 2025 katika kaunti hii ni hatua muhimu katika mapambano dhidi ya TB, ugonjwa ambao bado ni tishio kubwa kwa afya ya umma. Siku ya Kifua Kikuu Duniani huadhimishwa kila mwaka tarehe 24 Machi ili kuongeza uelewaku kuhusu magonjwa ya kuambukiza. Kaulimbiu ya mwaka huu, “Ndio! Tunaweza Kutokeza TB: Kujitolea, Kuwekeza, Kutekeleza,” ni wito thabiti wa matumaini, uharaka, na uwajibikaji katika vita dhidi ya ugonjwa huu. Mashine hii mpya ya eksirei ya kidijitali, yenye teknolojia ya hali ya juu ya kujiedesha na programu ya Computer-Aided Detection (CAD) iliyosakinishwa awali, inatarajiwa kuleta mapinduzi katika juhudi za uchunguzi wa TB katika kaunti hii. Uwezo wake mkubwa wa kufasiri picha za

X-Ray kwa usahihi unarahisisha utambuzi na kuharakisha matibabu. Akizungumza wakati wa maadhimisho hayo mjini Kutus, Waziri wa Huduma za Matibabu, Afya ya Umma, na Usafi wa kaunti (CEMC), George Karoki, alieleza imani yake kuhusu mchango wa teknolojia hii mpya katika kuhibiti maambukizi ya TB. “X-Ray hii inayotumia AI ni ya kubebeka, hivyo tunaweza kuipeleka kwenye maeneo yenye maambukizi mengi ya TB na vijijini, tukileta huduma za utambuzi karibu na wananchi,” alisema Karoki. Alisema huduma za uchunguzi wa TB zilizoimarishwa katika kaunti hii zimesababisha matokeo bora, ambapo kesi 1,597 ziligunduliwa 2024, ikilinganishwa na 1,516 mwaka wa 2023. Aliongeza kuwa ujio wa teknolojia na vifaa vipya unatarajiwa kuleta matokeo bora zaidi. Gavana Anne Waiguru, katika ujumbe wake wakati wa maadhimisho hayo, alisisitiza dhamira ya serikali yake katika kupunguza visa vya TB katika kaunti. “TB bado ni moja ya sababu kuu za vifo miongoni mwa watu wanaoishi na HIV,” alisema.



KENYATTA UNIVERSITY TEACHING, REFERRAL & RESEARCH HOSPITAL (KUTRRH)

P.O. Box 7674-00100 GPO NAIROBI TELEPHONE: 1558
EMAIL: info@kutrrh.go.ke



OPEN NATIONAL TENDER

Kenyatta University Teaching, Referral and Research Hospital invites sealed tender from interested eligible bidders as per the instructions provided here under.

No	Reference	Description Of Tenders	Closing Date	Eligibility
1.	KUTRRH/TNDR/G/016/F/2024-2025	Tender for Supply and Delivery of Fuels	10/4/2025 at 10.00am	Open
2.	KUTRRH/TNDR/G/014/SDIME/2024-2025	Tender for the Supply, Delivery Installation and Testing of Medical Equipment	10/4/2025 at 10.00am	Open
3.	KUTRRH/TND/G/015/SDLC/2024-2025	Tender for the Supply and Delivery of Laboratory Consumables	10/4/2025 at 10.00am	Open

Interested eligible candidates may obtain further information from our website: www.kutrrh.go.ke. All tenders **MUST** be submitted on or before the **STIPULATED RESPECTIVE DATES ABOVE at 10:00am.**

Bidders seeking clarification **MUST** strictly do so through the emails provided – procurement@kutrrh.go.ke. Any addendum issued will be sent to all the bidders and posted on the website (bidders are encouraged to keep visiting the website www.kutrrh.go.ke from time to time).

NOTE: Canvassing will lead to automatic disqualification.



FINANCIAL INCLUSION FUND (HUSTLER FUND)

KIBT Building (Ojjo Rd) 4TH Floor.
P.O Box 30547-00100 Nairobi.

Email: info@hustlerfund.go.ke, Website: hustlerfund.go.ke

PUBLIC NOTICE ON PUBLIC PARTICIPATION

The Financial Inclusion Fund was established under The Public Finance Management (Financial Inclusion Fund) Regulations, 2022. The main objective of the Fund is to offer viable financial products and services to the people at the bottom of the economic pyramid.

The Fund has developed its Draft Financial Inclusion Strategic Plan (2023-2027) which can be accessed and downloaded at www.hustlerfund.go.ke

Guided by Article 10 of the Constitution of Kenya that enshrines public participation as a national value, the Fund through this notice, hereby invites members of public and stakeholders to provide comments and feedback on the Draft Financial Inclusion Strategic Plan. The youth, women, persons with disabilities and other vulnerable groups are encouraged to participate.

Written submissions should be clearly marked “**Submission of Comments on the Draft Financial Inclusion Fund Strategic Plan (2023-2027)**” and submitted not later than **16th April, 2025** through email address pmad@hustlerfund.go.ke and copied to janetmeiseiyeki@gmail.com

Physical copies may also be hand-delivered to the following address

**Ag. Chief Executive Officer
The Financial Inclusion Fund
KIBT Building (Ojjo Road) 3rd Floor,
P.O Box 30547-00100 NAIROBI.**



Kenya kupunguza uagizaji chakula kwa mpango wa unyunyiziaji wa Sh598b

NA WANGARI NDIRANGU, KNA

Serikali itakusanya rasimilali zenye thamani ya Sh598 bilioni ili kupanua eneo la umwagiliaji kwa ekari milioni moja katika kipindi cha miaka 10 ijayo kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa chakula. Chini ya Mpango wa Kitaifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Umwagiliaji wa Miaka 10 (NISIP), serikali inalenga kuharakisha mikakati mbalimbali, ikiwemo ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi, dhamana za mikopo kwa wakulima wadogo, na kukuza kilimo cha kibiashara. Akizungumza na vyombo vya habari wakati wa hafla ya kabla ya uzinduzi, Katibu wa Idara ya Umwagiliaji, Ephantus Kimotho, alibainisha kuwa kuongeza uwekezaji katika sekta hiyo kutasaidia nchi kujitosheleza kwa chakula, hivyo kupunguza uagizaji wa chakula kutoka nje. Kimotho alieleza kuwa asilimia 39 ya rasilmali zinazohitajika zita-fadhiliwa na serikali



Katibu wa Unyunyiziaji Ephantus Kimotho wakati wa maonyesho kabla ya uzinduzi wa National Irrigation Sector Investment Plan (NISIP) katika KICC Machi 20, 2025.

pamoja na washirika wa maendeleo, huku asilimia 61 zikitarajiwa kutoka kwa sekta binafsi. “Mkakati huu unalenga kuwekeza katika umwagiliaji kwa ajili ya uzalishaji wa chakula na malisho na utaongozwa na njia tano za uwekezaji, kuwezesha vyanzo vingi vya ufadhili na mipango ya ndani inayolingana kimkakati na malengo ya serikali,” alisema. Kimotho aliongeza kuwa kwa sasa nchi ina ekari 747,000 chini ya umwagil-

iaji, ambapo ekari 83,000 zimeendelezwa katika miaka miwili iliyopita, hali ambayo imesababisha ongezeko la uzalishaji, hasa katika mnyororo wa thamani wa mpunga. “Hapo awali tulikuwa tukizalisha tani 192,000 za mpunga, lakini kutokana na ongezeko la ekari na miradi ya umwagiliaji, hasa katika mipango ya umma, uzalishaji wa mpunga umeongezeka hadi tani 293,000, ongezeko la asilimia 50,” alisema.

“Ifikapo mwaka 2027, tunalenga kuongeza uzalishaji hadi tani 440,000, na kufikia mwaka 2032, tani milioni moja,” aliongeza. Katibu huyo alibainisha kuwa Mpango wa Umwagiliaji wa Mwea ume-panuka kutoka ekari 25,000 hadi ekari 35,000, huku serikali ikihakikisha kuwa kilimo cha misimu miwili kinafanyika

kwa ufanisi, maji yana-patikana, na wakulima wanashughulikia matengenezo ya uendeshaji kwa asilimia 100. Aidha, serikali inapanga kuweka ekari 200,000 chini ya umwagiliaji katika eneo la Galana-Kulalu licha ya changamoto za mara kwa mara za uhaba wa maji. Kimotho alisema NISIP itafanya kazi na waunganishaji wa mazao ambao wamekuwa na changamoto ya kupata ubora na wingi unaohitajika wa mazao. “Mpango huu tunaojaribu kuunda ni mfumo wa

jinsi tunavyoweza kuunda kiunganishi kati ya waunganishaji wa mazao na wakulima ili wakulima waweze kupata mikataba ya kilimo na hivyo kuwa na kipato cha uhakika,” alisema. Vincent Kabuti, Katibu wa Umwagiliaji katika Wizara ya Maji, Usafi wa Maz-ingira, na Umwagiliaji, alisema lengo la mpango huu wa uwekezaji ni kuleta mapinduzi katika sekta ya umwagiliaji huku wakihakikisha wakulima wanapata mapato yaliyoimarika.



KENYA PIPELINE COMPANY LIMITED

Africa's Premier Oil & Gas Company



KENPIPE PLAZA,
SEKONDI ROAD,
OFF NANYUKI ROAD,
INDUSTRIAL AREA,
NAIROBI, KENYA.
P.O.Box 73442 - 00200,
TELEPHONE: 0709 723 000
(Call Center)
E-mail: Info@kpc.co.ke

INVITATION TO TENDER

Kenya Pipeline Company Limited invites tenders from eligible candidates for the following:

NO.	TENDER REFERENCE & DESCRIPTION	TENDER SECURITY	PRE-BID CONFERENCE DATES	SITE VISIT	CLOSING DATE
OPEN NATIONAL TENDER					
1.	KPC/PU/OT -198/FIN/NBI/24 - 25 Provision of Insurance Brokerage Services for the Period 1 st July 2025 to 30 th June 2028	KES.500,000.00	16-04-2025	N/A	23-04-2025
2.	KPC/PU/OT - 178/MECH/NBI/24 - 25 Modification of Truck Loading Facilities at PS25 - Nakuru Truck Loading System	KES.200,000.00	17-04-2025	15-04-2025	24-04-2025
The Tender documents can be viewed and downloaded from the website www.kpc.co.ke at no cost. Bidders will be required to register their companies on KPC SRM portal and send ONLY queries to opentender@kpc.co.ke. In addition, all addenda will be posted to those bidders who indicate their intention to participate through the SRM portal. No other email addresses shall be used and KPC shall not be liable if bidders choose to send their queries to other email addresses.					
FRAMEWORK					
3.	KPC/PU/FW-152(I&C)NBI/24-25 Framework contract for Provision of Maintenance Services for Automatic Tank Gauging (ATG) for a Period of Two Years	N/A	09-04-2025	N/A	16-04-2025
4.	KPC/PU/FW-193(CORR)NBI/24-25 Framework contract for Disposal of Petroleum Sludge for a Period of Two Years	N/A	09-04-2025	N/A	16-04-2025
The Tender documents can be viewed and downloaded from the website www.kpc.co.ke at no cost. Bidders will be required to register their companies on KPC SRM portal and send ONLY queries to technicalprocurement@kpc.co.ke. In addition, all addenda will be posted to those bidders who indicate their intention to participate through the SRM portal. No other email addresses shall be used and KPC shall not be liable if bidders choose to send their queries to other email addresses.					
NOTE: Bidders who are not registered in KPC SRM System should first register using this link https://e-procurement.kpc.co.ke/irj/portal					

Pre-bid conference will be held online as per the specified dates via the link provided in the tender document.

All bidders will be required to submit the tenders online via SRM Portal <https://e-procurement.kpc.co.ke/irj/portal> and all documents **MUST** be uploaded to the **COLLABORATION FOLDER**. Bidders shall not attach their documents at any other tab of the portal. To be received on or before the indicated closing date at **10.00 a.m.**

(NO BIDS WILL BE ACCEPTED IN THE TENDER BOX EXCEPT FOR THE ORIGINAL TENDER SECURITY)
Opening of the tenders will take place at **10.30 a.m.**

**GENERAL MANAGER (SUPPLY CHAIN)
FOR: MANAGING DIRECTOR**



PUBLIC SERVICE COMMISSION

Our Vision
“A citizen-centric public service”

Our Mission
“To reform and transform the public service for efficient and effective service delivery”

NOTICE

PUBLIC PARTICIPATION AND RECEIPT OF WRITTEN MEMORANDA ON: -

THE DRAFT PUBLIC SERVICE COMMISSION (AFFIRMATIVE ACTION) REGULATIONS, 2025

The Public Service Commission, pursuant to the provisions of Section 48 and 92 of the Public Service Commission Act, 2017, has developed **Draft Public Service Commission (Affirmative Action) Regulations, 2025.**

The Affirmative Action Draft Regulations is aimed at giving effect to the Constitutional requirement regarding inclusivity in terms of gender, Kenya's diverse communities, Persons with Disabilities and the youth in the public service.

The Commission, therefore seeks to invite stakeholders and the public in general to submit their views through written memoranda on the said regulations.

Written Memoranda may be sent to **the Secretary, Public Service Commission, P.O. Box 30095-00100, Nairobi;** hand-delivered to the Public Service Commission, Commission House, Harambee Avenue, or emailed to the secretary@publicservice.go.ke and, or legalservices@publicservice.go.ke to be received on or before **Friday, 2nd May, 2025.**

The **Draft Public Service Commission (Affirmative Action) Regulations, 2025** can be accessed from the Commission's website <https://www.publicservice.go.ke>, under **Publications-Legislation.**

**The Secretary/CEO
Public Service Commission
Commission House, Harambee Avenue
P.O. Box 30095-00100 NAIROBI**



Tume ya PSC yaanzisha mafunzo ya maadili kwa wafanyakazi wake

NA TOM MUEMA, PSC

Tume ya Huduma za Umma imeanza mchakato wa kubadilisha sekta ya utumishi wa umma ili kuzuia mazoea yasiyo ya maadili yanayodhoofisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Akizungumza katika hafla ya kufunga mpango wa wiki moja wa kuwahamasisha wafanyakazi wa Tume kuhusu maadili, thamani, na kanuni za utumishi wa umma, Makamu Mwenyekiti mpya, Mary Kimonye, alisisitiza kujitolea kwa Tume katika kushughulikia



Naibu Mwenyekiti wa PSC Mary Kimonye wakati wa semina ya kuhamasisha wafanyakazi wa tume hiyo kuhusu maadili

masuala ya uadilifu mdogo na kupungua kwa imani ya umma

katika utumishi wa umma. “Taswira iliyo huko nje ni kwamba utumishi wa umma umejaa ufasidi, na njukumu letu kubadilisha mtazamo huo. Mabadiliko yanaanza na kila mmoja wetu,” alisema Bi. Kimonye. Alisisitiza kuwa mageuzi lazima yaanze ndani ya Tume ili kuweka viwango bora vya utendaji kabla ya kupanua mabadiliko hayo katika sekta nzima ya utumishi wa umma. “Lengo letu kuu ni kubadilisha utumishi wa umma mzima uwe na ufanisi, tija, na uele-

kevu kwa mahitaji ya umma, kulingana na mamlaka yetu kama Tume. Tumejizatiti katika dhamira hii, ndiyo maana tunawahamasisha wafanyakazi wetu kuhusu maadili, thamani, na kanuni za utumishi wa umma,” alieleza kwa kusisitiza. Katibu/ Afisa Mtendaji Mkuu wa PSC, Bw. Paul Famba, alibainisha kuwa zoezi hilo la uhamasishaji ni mojawapo ya mikakati ya mageuzi inayolenga kuboresha Tume. Zoezi hilo la uhamasishaji wa ndani liliendeshwa na

kamati ya maadili chini ya uongozi wa Kamishna Mwanamaka Mabruki. Wakati huohuo, Tume imeboresha tovuti yake ya nafasi za kazi kwa kuboresha utendaji wake ili kurahisisha mchakato wa ajira. Tovuti mpya itakubali maombi kutoka kwa waombaji tu wanaokidhi sifa zilizobainishwa. Kulingana na Mkurugenzi wa Mifumo ya Taarifa za Usimamizi wa PSC, Harry Ruhia, jukwaa hilo lililoboreshwa litapunguza kwa kiasi kikubwa muda unaohitajika kuchuja waombaji.



REPUBLIC OF KENYA

MINISTRY OF DEFENCE

AUCTION NOTICE

1.

The Ministry of Defence (MOD) will sell by Public Auction Casted Vehicles, Equipment and General stores through the following tenders: -

MOD/423(0701) 2024/25

-

KNB Mtongwe (Mombasa Region)

MOD/423(0702) 2024/25

-

43 OCC (Nanyuki Region).

MOD/423(0703) 2024/25

-

DEFOD Kahawa (Nairobi Region).

MOD/423(0704) 2024/25

-

23 OCC Lanet (Nakuru Region).

2.

The goods will be sold on **‘as – is – where – is’** basis.

3.

The vehicles, equipment and boarded general stores can be viewed from 7 April 2025 during working days only (Monday to Friday) except on public holidays in Nairobi region (DEFOD - Kahawa, 12 Engrs – Thika, 23 OCC - Lanet, Nanyuki region (43 OCC) and Coastal Region (Kenya Navy Base Mtongwe and Mariakani Garrison) starting from 9:00 am to 4:00 pm after purchasing the catalogue as follows:

Tender No	Viewing Locations	Viewing Dates	Auctioneer's Name
MOD/423(0701) 2024/25	KNB Mtongwe	07 - 25 Apr 25	M/S Garam Auctioneers
MOD/423(0702) 2024/25	43 OCC Nanyuki	07 - 25 Apr 25	M/S View Line Auctioneers
MOD/423(0704) 2024/25	23 OCC Lanet	07 - 25 Apr 25	M/S J K Wanderi Auctioneers
MOD/423(0703) 2024/25	DEFOD Kahawa	07 - 25 Apr 25	M/S Philips Auctioneers

4.

Catalogues giving full details of items may be obtained on viewing days from the following offices upon payment of a non – refundable fee of KSh 1,000.00 (One Thousand Shillings) per set at:

a.

Ulinzi house main gate along Lenana road.

b.

23 OCC, Lanet.

c.

43 OCC, Nanyuki.

d.

KNB Mtongwe.

e.

DEFOD, Kahawa.

5.

Interested bidders will be required to pay a refundable bid number deposit of KSh 50,000.00 and KSh 30,000.00 for vehicles/equipment and stores respectively in cash payable to Ministry of Defence before the last day of viewing. Each Bid number will only be allowed to bid for one Lot ONLY. Original catalogue and receipts for both the catalogue and bid number deposits will be presented at the entrance for one to be allowed to participate in the auction.

6.

The Public Auction will be undertaken at the following sale yards on the dates indicated against each:

a.

MOD/423(0701) 2024/2025

-

KNB Mtongwe

-

29 Apr 25 at 10:00 am.

b.

MOD/423(0702) 2024/2025

-

43 OCC Nanyuki

-

06 May 25 at 10:00 am.

c.

MOD/423(0704) 2024/22025

-

23 OCC Lanet

-

13 May 25 at 10:00 am.

d.

MOD/423(0703) 2024/2025

-

DEFOD Kahawa

-

20 May 25 at 10:00 am.

7.

All successful bidders will be required to pay a deposit of 25% of the bid at the fall of the hammer and the remaining balance within fourteen (14) days after the auction, failure to which the award will be cancelled and the deposit forfeited.

8.

Unsuccessful bidders will be refunded the bid number deposits on presentation of the respective original receipts.

9.

Successful bidders tender bid deposit will be credited to his/her bid price and thereafter he/she will be required to top up the difference thereof.

10.

Successful bidders will be required to collect their item(s) within thirty (30) days after making full payment failure to which they will be liable to pay storage charges at a rate of 1% of bid offer per day up to a maximum of three (3) months. Items not collected within the three (3) months will be forfeited together with the monies paid against them.

11.

Successful bidders will be responsible for payment of duty, VAT and other related charges, where applicable, as established under Government regulations.

12.

The sale is subject to a Reserve Price.

13.

Ministry of Defence reserves the right to reject any bid below the reserve price and does not bind itself to give the reasons for the rejection.

14.

Bidders who will purchase motor vehicle(s) will be required to ensure that the vehicles are painted with non-military colour patterns (where applicable) before being put on the road.

15.

No EX – Military vehicle should be put on the road with EX – Military number plates contrary to which the vehicle will be impounded immediately.

16.

All successful bidders must get clearance from KRA before collection of the items from the sale yards.

Head of Supply Chain Management
for Principal Secretary





REPUBLIC OF KENYA

MINISTRY OF ENERGY AND PETROLEUM

STATE DEPARTMENT FOR ENERGY

INVITATION TO TENDER

REHABILITATION & CORRECTIVE MAINTENANCE OF SOLAR PV SYSTEMS IN 46 NUMBER SCHOOLS, HEALTH FACILITIES, POLICE STATIONS/POSTS, ADMINISTRATIVE, COUNTY & SUB-COUNTY OFFICES IN ASAL COUNTIES (RE-TENDER)

TENDER NO. MOEP/SDE/ONT/07/2024-2025

1.

The Ministry of Energy & Petroleum, State Department for Energy invites sealed tenders from eligible candidates for **REHABILITATION & CORRECTIVE MAINTENANCE OF SOLAR PV SYSTEMS IN 46 NUMBER SCHOOLS, HEALTH FACILITIES, POLICE STATIONS/POSTS, ADMINISTRATIVE, COUNTY & SUB-COUNTY OFFICES IN ASALS DISTRICTS/COUNTIES (RE-TENDER).**

2.

Tendering will be conducted under Open National Tendering Method and is open to all qualified and interested Tenderers using a standardized tender document. Tenderers will be allowed to tender for one or more lots.

3.

Qualified and interested tenderers may obtain further information and inspect the Tender Documents during office hours 0900 to 1700 hours at the address given below.

4.

A complete set of tender documents may be obtained by interested tenderers electronically from the State Department for Energy Website www.energy.go.ke or tenderers' portal www.tenders.go.ke. Tender documents obtained electronically will be **free of charge**.

5.

Tender documents may be viewed and downloaded for free from the website www.energy.go.ke. Tenderers who download the tender document must forward their particulars immediately to Supply.Chain@energy.go.ke, address - **Ministry of Energy and Petroleum, State Department for Energy, South C, Kawi Complex, Block A, 1st floor, Procurement office, P.O. Box 30582-00100, Nairobi** to facilitate any further clarification or addendum

6.

Tenders shall be quoted in Kenya Shillings and shall include all taxes. Tenders shall remain valid for (154) days from the date of opening of tenders.

7.

The Tenderer shall chronologically serialize all pages of the tender documents submitted. The Tender documents should be either hardbound or Tape-Bound.

8.

Completed tenders must be delivered to the address below on or before **09th April, 2025 at 10.00 A.M.** Electronic Tenders will not be permitted.

9.

Tenders will be opened immediately after the deadline date and time specified above or any dead line date and time specified later. Tenders will be publicly opened in the presence of the Tenderers' designated representatives who choose to attend at the address below.

10.

Late tenders will be rejected.

11.

The addresses referred to above are:

A.

Address for obtaining further information
The Principal Secretary
State Department for Energy
Ministry of Energy and Petroleum,
Nairobi South C, Kawi Complex, Block A,
1st floor Procurement office
P.O. Box 30582-00100, Nairobi
Head, Supply Chain Management Services,
email supply.chain@energy.go.ke

B.

Address for Submission of Tenders.
State Department for Energy
Ministry of Energy and Petroleum,
P.O. Box 30582-00100, Nairobi
Nairobi South C, Kawi Complex, Block A,
and to be Deposited in the Tender Box on Ground floor at the entrance of Kawi House Block 'A'

C.

Address for Opening of Tenders.
State Department for Energy, Ministry of Energy and Petroleum
Nairobi South C, Kawi Complex, Block A, 3rd floor meeting room

PRINCIPAL SECRETARY
STATE DEPARTMENT FOR ENERGY



Owalo asifia mradi wa unyunyiziaji wa Maragua kama ufanisi mkubwa



Naibu Mkuu wa Wafanyakazi, Utendakazi na Ufuatiliaji Matokeo katika Afisi ya Rais Eliud Owalo aongoza kundi la maafisa serikalini kukagua mradi wa Unyunyiziaji Maji wa Maragua Ridge.

NA BERNARD MUNYAO, KNA

Serikali kwa sasa inatekeleza mradi wa umwagiliaji katika Maragua Ridge, Kaunti ya Murang'a, ambao unawanufaisha kaya 848. Mradi huu, ambao umegharimu Sh312 milioni, umekamilika kwa asilimia 99 na utahudumia ekari 400 katika maeneo ya wadi za Kambiti na Kamahuha ndani ya eneo bunge la Maragua. Kwa sasa, eneo hili linategemea kilimo cha mvua, lakini mradi huu wa umwagiliaji unatarajiwa kubadilisha maisha ya wakazi wa eneo hilo na hivyo kuimarisha usalama wa chakula. Naibu Mkuu wa Wafanyakazi anayesimamia Utendaji na Utekelezaji katika Ofisi ya Rais, Eliud Owalo, alipoteembelea mradi huo, alisema kuwa baadhi ya wakulima tayari wanapata maji kwa ajili ya umwagiliaji mashambani mwao. Owalo alisisitiza umuhimu wa mradi huu, akisema kuwa utaimarisha maisha ya wakazi kupitia kilimo cha umwagiliaji huku pia ukiwawezesha kupata maji kwa matumizi ya nyumbani. Aliwahimiza wakulima kujipanga vyema na kuingia katika kilimo cha kibiashara ili kupata mapato kutoka kwa ardhi yao. "Mradi huu wa umwagiliaji utaleta mabadiliko makubwa. Wakulima wanapaswa kuwa na mpangilio mzuri ili kupata msaada wa serikali, hususan katika huduma za ugani na upatikanaji wa masoko. Hii ita-



Eliud Owalo akagua mradi wa Maragua Ridge katika kaunti ya Murang'a.

hakikisha uchumi wa vijijini unakuwa imara na pesa zinasambaa katika ngazi za mashinani," alisema Owalo, aliyekuwa ameandamana na Kamishna wa Kaunti ya Murang'a, Joshua Nkanatha. Katika mradi huu unatekelezwa na Mam-laka ya Umwagiliaji ya Kitaifa (NIA), wakulima 400 tayari wameunganishwa na mfumo wa umwagiliaji, huku zaidi ya ajira 12,700 zikiwa zimebuniwa kupitia mradi huo. Owalo alisema kuwa mradi huu wa umwagiliaji ni wa gharama nafuu kifedha, kijamii na kiuchumi, akiongeza kuwa utajigharimia ndani ya kipindi cha miaka minne. Alisema kuwa mradi huu unatarajiwa kuimarisha usalama wa chakula na kukuza uchumi, huku ukiwawezesha wakulima kulima matunda, mboga, mahindi na maharagwe mwaka mzima.

